# KISWAHIKI 102
# MTIHANI WA KWANZA MUHULA WA PILI
# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**MUDA: SAA 2:00**

**SEHEMU YA A: UFAHAMU (ALAMA 15)**

a) MAKARIBISHO YA SHULE YA UPILI/ SHULE YA UPILI (1x1=1)

b) Ilikuwa siku yao ya kwanza katika shule ya upili na walikuwa wakingoja hotuba ya mwalimu mkuu (1x1=1)

c) kukaribishwa rasmi na mwalimu mkuu
kujulishwa na kufahamishwa mambo kadha (2x1=2)

d) wawe na nidhamu
wasiwe na furaha sana
watulie haraka katika mazingira mapya (2x1=2)

e) kijengacho mtu ni utu na tabia
hufaulisha mtu maishani (2x1=2)

f) umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
Tamu ikizidi tamu huwa si tamu tena
Ukilima pantosha,utavuna pankwisha (2x1=2)

g) kuku akitamia mayai vizuri huangua vifaranga sawa na mwanafunzi anayetia bidii masomoni anavyofaulu katika mitihani yake. (1x2=2)

h) Eleza maana;

Viranja; wanafunzi viongozi
Tarakilishi; kompyuta
aina ya mashine ya teknolojia ya habari na mawasiliano
Maabara; jumba/chumba cha uchunguzi wa kisayansi (3x1=3)

**SEHEMU B: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Konsonanti; sauti ambazo hewa huzuiliwa katika ala za kutamkia zinapotamkwa

Irabu; sauti ambazo hutamkwa kwa ulaini/ bila hewa kuzuiliwa katia ala za kutamkia (2x 1=2)

b) ala tuli; ala zisizosonga wakati wa kutamka kwa mfano, meno, kaakaa gumu, kaakaa kaini, ufizi
ala sogezi; ala zinazosonga wakati wa kutamka kwa mfano midomo, ulimi (2x1=2)

c)

i) sauti ghuna ; sauti ambazo husababisha mtetemeko wa nyuzi za sauti zinapotamkwa



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

sauti sighuna; sauti zisizosababisha mtetemeko wa nyuzi za sauti wakati wa kuzitamka. (2x1=2)

ii) Onyesha sauti ghuna au sighuna kati ya hizi ulizopewa.

/k/: sighuna
/g/;ghuna
/s/: sighuna
/z/;ghuna (4x½=2)

d) i) Tamko moja katika neno/Pigo moja la sauti katika neno (1x2=2)
ii) Silabi wazi, silabi funge (2x1=2)
iii). I; o-a
K ; a-l-ha-mi-si
KI; ma-ma
KKI; ndo-a
KKKI; mbwe-ha (2x1=2)
(kadiria mifano ya maneno)

e) Eleza maana;
i) Kiimbo; kupanda na kushuka kwa sauti wakati wa kutamka
ii) Shadda; mkazo unaowekwa katika silabi fulani ya neno (2x1=2)

f)

i) /a/; irabu ya chini, kati, hutamkwa midomo ikitandazwa
ii) /p/; kipasuo, sighuna, hutamkwa midomoni (6 x ½=3)

g) Taja na ueleze aina nane za maneno ya Kiswahili

- ✓ **Nomino** Neno linalotaja kiumbe, kitu, hali, mahali, tendo, dhana, n.k. Kuna aina 6 za nomino.
- ✓ **Vitenzi**Kitenzi ni neno linaloeleza kuhusu jambo linalofanywa. Kuna aina tano za vitenzi vya Kiswahili.
- ✓ **Viwakilishi**; viambishi au maneno yanayotumiwa badala ya nomino.
- ✓ **Vivumishi**; maneno yanayotoa habari zaidi kuhusu nomino.
- ✓ **Vielezi (E)**Viambishi au maneno yanayoeleza zaidi kuhusu kivumishi, kitenzi au kielezi kingine.
- ✓ **Viunganishi;**Neno au fungu la maneno la kuunganishia maneno,kikundi cha maneno,kishazi,kirai au sentensi.
- ✓ **Vihusishi;** Maneno yanayoonyesha uhusiano.
- ✓ **Vihisishi;** Maneno yanayotoa hisia za moyoni.

(8x½=4)

h) Tambua aina za maneno katika sentensi ifuatayo:

Mwerevu sana anapumzika <u>chini ya</u> mti jijini
W E T H N E (6 x ½=3)

i) Gari lile bovu ; kundi nomino
liliondolewa barabarani; kundi tenzi (2 x 1=2)

j) KI-VI; Kitabu **ki**mepotea/ Viti **vi**mepotea
LI-YA; Gari **li**mebingiria/ Magari **ya**mebingiria



Teacher.co.ke
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

U-ZI; Ubao **u**mepasuka/ Mbao **zi**mepasuka (1 x 3=3)

k) Walimu hawakununua karatasi na kalamu (1 x 2=2)

l) i) Kirai ni fungu la maneno lisilo na maana kamili (1x1=1)

ii) Darasa letu; kirai nomino
lina wanafunzi ; kirai kitenzi
watiifu sana; kirai kivumishi (3 x 1=3)

m) Toto limeabiri jigari leo asubuhi (1 x 2=2/0)

n) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu (1 x 1=1)

**SEHEMU YA C: ISIMU JAMII (alama 10)**

**a) Lugha** ni mfumo wa sauti nasibu unaotumiwa na binadamu kuwasiliana. (1x1=1)

**b) Kiswahili kama lugha**

i. Ni mali ya mwanadamu
ii. kimekua na kubadilika katika kipindi kirefu
iii. Kiswahili kina utamaduni wake
iv. Kiswahili kina sheria na kaida zake
v. Kiswahili huwa na sauti na ishara zake
vi. Kiswahili huathiriana na lugha nyingine (4x1=4)

**c) Umuhimu wa Kiswahili**

1. Ni chombo cha mawasiliano
2. Ni kitambulisho cha mtu na utamaduni wake.
3. Huunganisha /huleta umoja wa wanajamii
4. Hutumiwa kuelimisha/kutoa elimu
5. Ni chombo cha burudani kv nyimbo,shairri,michezo ya kuigiza.
6. Ni chombo cha utawala;serikali huitumia kupasha sera zake
7. Inatumiwa kuendeleza biashara
8. Inatumiwa kuendeleza dini. (5x1=5)

**SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI (alama 15)**

a) **Fasihi simulizi**

Fasihi inayowasiolishwa kwa njia ya mdomo. (1x2=2)

**b) Umuhimu wa Fasihi Simulizi katika jamii**

- ✓ Kuburudisha/kustarehesha/kufurahisha/ kuchangamsha/kusisimua na kupumbaza akili na kiwiliwili – ujumbe huwasilishwa kwa njia ya kuvutia na kuleta ucheshi
- ✓ Kuadilisha /kufunza maadili kwa wanajamii kwa kuwahimiza kuiga sifa chanya na kukataa sifa hasi za wahusika.
- ✓ Kukuza uwezo wa kufikiri/kudadisi k.m vitendawili na chemshabongo.
- ✓ Kuhifadhi historia ya jamii k.m. mighani, visaviini, mapisi, tarihi n.k.hizi hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.



Teacher.co.ke
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

- ✓ Kukejeli tabia zinazokiuka matarajio ya jamii k.v soga, methali, n.k.
- ✓ Kuendeleza tamaduni za jamii kwani husawiri imani na desturi za jamii. k.v kitendawili 'Nyumbani mwetu mna papai lililoiva lakini siwezi kulichuma.' - Mtu hawezi kumwoa dadake.
- ✓ Kuunganisha watu pamoja kwa kuwajumuisha pamoja wakati wa ngoma, kuimba, utambaji, n.k.
- ✓ Kukuza lugha k.v. ulumbi na misimu inapokita kimatumizi na kujumuishwa katika lugha sanifu.
- ✓ Kukuza ubunifu k.v. malumbano ya utani, vitanza, ndimi ngonjera, n.k.
- ✓ Kukuza uzalendo kwa kufanya wanajamii kuonea fahari jamii zao na kuiga mashujaa au watu waliotendea jamii makuu.
- ✓ Kuonya na kutahadharisha wanajamii dhidi ya tabia hasi k.v. ulafi, uchoyo, n.k

(za kwanza 5x1=5)

c) **Tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi/sifa za fasihi simulizi/zinazofanya utanzu uwe wa fasihi simulizi**

- ✓ Fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo ilhali fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi.
- ✓ Fasihi simulizi huhifadhiwa akilini ilhali fasihi aandishi huhifadhiwa kwa maandishi.
- ✓ Fasihi simulizi ni mali ya jamii ilhali fasihi andishi ni mali ya mtu binafsi/mwandishi.
- ✓ Fasihi simulizi ina wahusika wa kila aina k.v binadamu, wanyama na ndege, mazimwi na majitu, miungu, mizimu, mashetani na vitu visivyo na uhai k.v. mawe na miti ilhali fasihi andishi ina wahusika binadamu kwa kiasi kikubwa.
- ✓ Fasihi simulizi ina tanzu nyingi kuliko fasihi andishi.
- ✓ Uwasilishaji wa fasihi simulizi huweza kuandamana na utendaji k.v matumizi ya ishara, nyimbo, makofi, kuimba, kubeba zana katika majigambo n.k ilhali ule wa fasihi andishi hauandamani na utendaji isipokuwa inapowasilishwa mbele ya hadhira.
- ✓ Fasihi simulizi huwasilishwa mbele ya hadhira ilhali fasihi andishi si lazima iwasilishwe mbele ya hadhira.
- ✓ Fasihi simulizi huwasilishwa mahali maalum k.v jandoni, matangani, arusini, n.k ilhali fasihi andishi haina mahali maalum.
- ✓ Fasihi andishi huhitaji muda kutunga ilhali baadhi ya fasihi simulizi huzuka papo hapo k.m. semi, maigambo.
- ✓ Fasihi simulizi ina uwezo mkubwa wa kubadilishwa na fanani anapowasilisha ufaraguzi) bali fasihi andishi haibadiliki isipokuwa mwandishi aiandike upya.
- ✓ Fasihi simulizi ina historia ndefu kuliko fasihi andishi kwa kuwepo tangu mwanzo wa maisha ya binadamu
- ✓ Fasihi simulizi huwasilishwa wakati maalum k.v. usiku, kipindi fulani cha mwaka ilhali andishi haina wakati maalum.
- ✓ Hadhira ya fasihi simulizi huweza kuwasiliana moja kwa moja na mwasilishaji ilhali ile ya fasihi simulizi sio lazima iwasiliane na mwandishi.
- ✓ Hadhira ya fasihi simulizi ni kubwa kuliko ile ya fasihi andishi kwani huhusisha hata wasiojua kusoma na kuandika.
- ✓ Hadhira ya fasihi simulizi ni hai yaani inajulikana na fanani ilhali ile ya fasihi simulizi si hai yaani haijulikani na mwandishi.

(za kwanza 8x1=8)



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Teacher.co.ke